



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
MKOA WA MWANZA



Unapojibu tangazo hili tafadhali taja
Kumb. Na. AB.16/194/02/124

Tarehe: 15/02/2024.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WAKUSANYA MAPATO.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema anawatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi za kazi ya kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

1. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
- iii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- iv. Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
- v. Awe na mdhamini mwenye mali isiyo hamishika yenye thamani ya kuanzia Tshs 10,000,000/= (milioni kumi) na kuendelea, Dhamana ya mali isiyohamishika itathibitishwa kwa kuwasilisha Halmashauri hati au nyaraka ya umiliki inayotambulika na iliyothibitishwa kisheria kuwa ni mali ya mtoa dhamana.
- vi. Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai au kuhukumiwa kifungo jela katika mahakama yoyote.
- vii. Awe tayari kufanya kazi katika kata yoyote iliyoko ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.
- viii. Mtu yoyote aliyewahi kufanya kazi na halmashauri kisha kusababishia hasara ya upotevu wa mapato au kudaiwa na halmashauri **HARUHUSIWI KUOMBA KAZI YA KUKUSANYA MAPATO**

2. MAJUKUMU YA KUKUSANYA MAPATO.

- i. Kukusanya mapato ya halmashauri kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo katika eneo la wilaya ya Sengerema kwa kutumia mashine ya kielektroniki (POS).
- ii. Kuwasilisha benki kupitia akaunti ya mapato ya halmashauri makusanyo yote yaliyokusanywa ndani ya saa 24 katika siku za kazi au siku ya kwanza ya kazi ya wiki au baada ya sikukuu.


- iii. Kutoa risiti za mashine ya kielektroniki (POS) kiasi sawa na fedha atakayolipa mlipaji.
- iv. Kutunza vifaa vya kukusanya mapato (POS, rejista) na nyaraka za benki au Halmashauri zitakazothibitisha uingizaji wa fedha benki.
- v. Kufanya uhakiki kila siku wa makusanyo ya siku na taarifa ya mashine ya kukusanya mapato.
- vi. Kuwasilisha halmashauri mashine ya kukusanyia mapato (POS) kwa ajili ya uchunguzi.
- vii. Kufanya kazi nyingine zitakazohusu mapato kadri atakavyoelekezwa na mwajiri.

3. MALIPO YA KUKUSANYA MAPATO

Malipo ya kazi ya ukusanyaji mapato yatakuwa asilimia 5 (5%) ya makusanyo yaliyokusanywa na kuwasilisha benki ikijumlishwa na 60,000.00 kwa kila mwezi.

Maombi yote yatumwe/yaletwe kwa: -
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
S.L.P.175,
SENGEREMA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 29/02/2024 saa 9:30 Alasiri



Binuru M. Shekidele.

MKURUGENZI MTENDAJI (W),

SENGEREMA.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 175
SENGEREMA